JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO

SHULE YA SEKONDARI KWEMARAMBA
S.L.P 103 LUSHOTO
amiribakarikaniki@gmail.com
Website: www.sites.google.com/Site/kwemarambass/home
Tel: 0784834149/ 0654305653

KMB. Na KMSS/C/PS/V.1/2018/04

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2018/19 KATIKA SHULE YA SEKONDARI KWEMARAMBA Na. S1092

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguwa kujiunga na kidato cha tano mwaka 2018/19 katika shule ya Sekondari kwemaramba mchepuo wa**PCB/PCM** na **EGM.**

Shule ya sekondari kwemaramba ipo Wilaya ya **Lushoto** Tarafa ya **Mlalo** Mkoani **Tanga**. Umechaguliwa kutokana na kufaulu vizuri mitihani yako ya kidato cha nne2017, hivyo ukiwa kwemaramba unatakiwa kusoma kwa bidii na maarifa, ili utumie nafasi uliyopewa na jamii na serikali vizuri kwa manufaa yako, ya jamii na serikali. Ukiwa Kwemaramba Sekondari utalazimika kufuata sheria, kanuni na taratibu, na maadili ya uanafunzi, (sheria za shule zimeambatanishwa). Ukienda kinyume nasheria hizi, hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule kwani utovu wa nidhamu hautavumiliwa.

Utaripoti shuleni tarehe 02/07/2018 tayari kwa kuanza masomo na mwisho wa kuripoti ni tarehe 16/07/2018. Utajaza kiambatanisho A na B fomu ya kujua afya yako (**Medical Examination Form**) na ufike nazo shuleni siku ya kuripoti. Fika na nakala ya cheti cha kuzaliwa na kama huna nenda mahakamani ili upewe Affidavit kuonesha kuwa wewe ni raia wa Tanzania.

MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

Kila mwanafunzi ajishonee mwenyewe sare zifuatazo

1.1 Sare za shule kwa wavulana

1	**Suruali mbili (2) za darasani nyeusi zisizobana**
2	**Shati jeupe tetron special jozi mbili (2) ya mikono mirefu**
3	**Tai nyeusi kwa ajili ya darasani**
4	**Tracksuit za rangi ya blueu.**
5	**Boshori la kuvalia kichwani usiku rangi ya bendera ya taifa**
6	**Mikanda ya kawaida**

1.3 Masweta mawili ya shule bei nishilingi sh.30,000/= na T-shirt sh. 12,000/= zitapatikana shuleni.

N.B FEDHA HIZI ZISILIPWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE AJE NAZO MKONONI.

1.2 Sare za shule kwa wasichana

1	**Sketi mbili (2) nyeusi za darasani zinazovuka magoti na hijabu nyeupe ya heshima kwa ambao ni waislamu**
2	**Shati jeupe tetron special jozi mbili (2) mikono mirefu**
3	**Skafu nyeusi kwaajili ya darasani**
4	**Tracksuit za bluu.**
5	**Boshori la kuvalia kichwani usiku rangi ya bendera ya taifa**

1.3 Masweta mawili ya shule bei nishilingi sh.30,000/= na T-shirt sh. 12,000/= zitapatikana shuleni.

N.B FEDHA HIZI ZISILIPWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE AJE NAZO MKONONI.

1.4 Mahitaji anayotakiwa kuja nayo shuleni.

(i) Wavulana

(a) Suruali na shati (Kaunda suti) mikono mirefu za kushindia rangi ya Damu ya mzee jozi mbili (aje akiwa amevaa jozi moja)
(b) Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vya kufunga na kamba (visiwe buti au vyenye visigino virefu au bajaji) na soksi nyeusi
(c) Shuka 2 za rangi ya bluu bahari
(d) Blanketi au shuka nzito za kujifunika
(e) Picha 4 za passport size
(f) Chandarua
(g) Godoro nilakukodisha shuleni kwa shilingi 15,000 kwa muhula
(h) Sanduku imara la bati (tranka) kwaajili ya kuhifadhia vifaa vyako
(i) Jembe na mpini ,kwanja na fagio ya skwiza, mfagio laini wa ndani wa kusimama.
(j) Ndoo mbili ndogo kwa ajili ya maji kunywa na usafi wake binafsi
(k) Kijiko na sahani isiyo ya plastiki

(ii) Wasichana

(a) Gauni la kushindia la mikono mirefu rangi ya Damu ya mzee jozi mbili (aje akiwa amevaa jozi moja)
(b) Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vya kufunga na kamba (visiwe buti au vyenye visigino virefu au bajaji) ma soksi nyeupe
(c) Shuka 2 za rangi ya bluu bahari
(d) Blanketi au shuka nzito za kujifunika
(e) Picha 4 za passport size
(f) Chandarua
(g) Godoro ni lakukodisha shuleni kwa shilingi 15,000 kwa muhula
(h) Sanduku imara la buti (tranka) kwaajili ya kuhifadhia vifaa vyako
(i) Jembe na mpini ,kwanja na fagio ya skwiza, mfagio laini wa ndani wa kusimama.
(j) Ndoo mbili ndogo kwa ajili ya maji kwanywa na usafi wake binafsi
(k) Kijiko na sahaniisiyo ya plastiki

2. VIFAA VYA DARASANI

(a) Ufike na daftari za kutosha (kuanzia Counter book 12, Quire 3) kwa masomo yako utakayosoma, kalamu na mkebe (Mathematics Set)
(b) Kikokotoo cha sayansi na hisabati (scientific Calculator), na sio programmable calculator
(c) Spring file mbili za plastic
(d) Kwa masomo ya PCB na PCM aje **koti** la maabara
(e) kwa wale wa PCB pekee aje na dissecting kit 01

3. Ada na michango mingine itakayolipwa benki kwenye account ya shule ya sekondari kwemaramba namba 41603500041 NMB Lushoto.

	Ada kwa mwaka	**70,000**
	kuboresha taaluma kwa mwaka	**10,000**
	kitambulisho mara moja	**5,000**
	Mpishi kwa mwaka	**10,000**
	Karani kwa mwaka	**6,000**
	Mlinzi kwa mwaka	**10,000**
	Tahadhari na (hairudishi) mara moja	**5,000**
	Mchango wa dawati mara moja	**25,000**
	Kuimarisha miundombinu shuleni mara moja	**20,000**
	Kuchangia mahafali kidato cha sita kwa mwaka 2019	**10,000**
	Nembo ya shule (mara moja)	**2,000**
	Afya na huduma yakwanza kwa mwaka	**15,000**
	JUMLA	**188,000**

MUHIMU:

1. Mwanafunzi aje na risiti ya malipo bank pay in slip (**BPS**)
2. Mwanafunzi atapokelewa tu iwapo amekamilisha kulipa ada, michango mingine na kukabidhi vifaa vyote vilivyoagizwa.
3. Mwanafunzi anashauriwa kuwa awe na fedha za mfukoni (pocket money).
4. Kufika shuleni kwa haraka panda magari ya **Lushoto- Mlalo**.shuka kituo kinachoitwa MAJULAI Kisha panda boboda kwash. 1500 hadi shuleni.
5. Ukifika shuleni ripoti moja kwa moja kwa mkuu wa shule kisha taratibu nyingine zitafuata.
6. Hakikisha unasoma kwa makini maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.
7. Kila mwanafunzi aje na vitabu vinavyohusiana na tahasusi (combination) anayosoma.
8. Kila mwanafunzi ataleta rimu moja aina ya **Mondi No 1 Size A4**kwa kila muhula wa masomo.

TAMATI
KARIBUNI SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KWEMARAMBA

_____
AMIRI BAKARI KANIKI
MKUU WA SHULE

Mimi ……baba/mama/mlezi wa ……..

KIAMBATISHO B
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI KWEMARAMBA S.L.P 103, LUSHOTO
SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

1. HESHIMA

(a) Mwanafunzi atasimama kumsalimia mwalimu au mtu yoyote aliyemzidi umri anapopita anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
(b) Mwanafunzi atatumia lugha safi (inayokubalika) wakati wowote kati yake na wenzake na kwa watu wengine akiwa shuleni au nje ya shule.
(c) Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko kati yake na walezi wake.
(d) Mwanafunzi ataitika wito maramoja na kukimbilia aliiko mkuu anayemuuta.
(e) Mwanafunzi anapaswa kuheshimu kazi yoyote anayopewa na mwalimu au mlezi na anatakiwa ashirikiane na wenzake ili kuifanya kazi hiyo.
(f) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifana picha za viongozi wa serikali nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
(g) Mwanafunzi atasimamia katika mstari wakati wowote anaposubiri kupata huduma.
(h) Mwanafunzi atakaa kimya wakati wowote akiwa darasani, asitoke nje ya darasa au eneo la shule bila ruhusa ya mwalimu. Atatoka nje ya eneo la shule kwa siku zilizotangazwa au ruhusa.

2. MAHUDHURIO

(a) Mwanafunzi anatakiwa ahudhurie vipindi vyote vya darasani kwa muda wote wa masomo. Atatakiwa kufika shuleni kwa tarehe zote zilizopangwa na anapokosa kufika siku anapofika akatoe taarifa kwa mmojawapo wa hawa
    i. Mwalimu wa zamu wa siku hiyo
    ii. Mwalimu wa darasa
    iii. Makamu wa mkuu wa shule

(b) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule kamavile mabaraza ya shule, ukaguzi wa usafi, na kupandisha bendera ya Taifa.
(c) Mwanafunzi atatakiwa kuwahi shughuli zote shuleni kamazilivyopangwa kwenye ratiba ya shule. Tena anatakiwa kuwahi anapotakiwa au anaposikia kengele.
(d) Mwanafunzi anatakiwa kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yoteanayopewa na mwalimu wa somo darasani. Akikosa jaribio au mtihani wowote akamuone mwalimu wa somo na mwandamizi taaluma.

3. SARE YA SHULE NA USAFI

Mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare safi ya shule wakati wote wa saa za shule. Atakuwa na vazi tofauti pale tu atakapo agizwa kama vile nguo za michezo wakati wa michezo au nguo za kushindia. Shule yetu ina utaratibu wa wanafunzi wote kuwa na mavazi ya nje ya madarasa yaani shamba dress. Hivyo hairuhusiwi kabisa kwa mwanafunzi kuja shuleni na mavazi mengine ambayo siyo uniform na yasiyoruhusiwa shuleni. Ikiwa mwanao atakuja shuleni na mavazi zaidi ya yale yaliyoruhusiwa shuleni, yatakamatwa na hazitarudishwa

kamwe bali zitateketezwa. Hivyo ndugu mzazi mtoto wako anapofungasha sanduku lake mkague kabisa.

4. MAKATAZO

4.1 SEHEMU ASIZORUHUSIWA KUTEMBELEA MWANAFUNZI

(a) Mwanafunzi asitembee sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali au ruhusa:
   i. Ofisi ya walimu
   ii. Maabara
   iii. Nyumba za walimu na wafanyakazi
   iv. Chumba cha walimu au wafanyakazi

(b) Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutembea sehemu hizi:
   i. Vilabu vya pombe
   ii. Kumbi za starehe
   iii. Nyumba za kufikia wageni

(c) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa/kibali maalumu.

(d) Mwanafunzi hatakiwi kuonekana bwenini wakati wa darasani bila kibali cha patron au matron.

(e) Muda wa kusoma usiku (night preparation) ni kuanzia saa 1:30 jioni hadi saa 5:00 usiku na baada ya hapo taazote zitazimwa madarasani.

4.2 NI MARUFUKU

(a) Kuiba mali ya mtu binafsi au umma
(b) Kufanya uasherati, ubakaji au ushoga
(c) Kulewa kilevi cha aina yeyote au kuvuta sigara au bangi
(d) Kupiga au kupigana
(e) Kuharibu mali ya umma
(f) Kuoa au kuolewa
(g) Si ruhusa kwa wanafunzi kumiliki au kuwa na simu, kamera, radio na pasi shuleni. Iwapo mwanafunzi atapatikana na vitu hivyo hapa shuleni vitataifishwa na havitarudishwa kamwe na mwanafunzi atalazimika kufukuzwa shule endapo atapatikana na vitu hivyo. Ili kuepuka adha hiyo hakikisha kuwa humpi mwanao vitu hivyo visivyokubalika shuleni. Ili kurahisishwa mawasiliano, unaweza kumwandikia mwanao namba ya simu ambayo utaitumia akihitaji mawasiliano na mzazi au mlezi na atasaidiwa mawasiliano ya simu na ofisi ya mkuu wa shule kupitia namba zilizoorodheshwa hapo juu.

5. MAKOSA YANAYOMFUKUZISHA SHULE

(a) Uasherati, ubakaji, ushoga, kuoa au kuolewa.
(b) Wizi ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
(c) Kuvuta bangi.
(d) Kupiga au kupigana
(e) Kudharau bendera ya taifa na kuharibu mali ya umma.
(f) Kupata, kutoa mimba au kusababisha mimba shuleni au nje ya shule.
(g) Kugoma, kuongoza, kuchochea mgomo au vurugu, kuchafua amani au usalama wa watu.
(h) Kukashifu na kukataa adhabu halali
(i) Kutumia au kumiliki simu shuleni.
(j)

ANGALIZO

Ni jukumu la mwanafunzi kufauata sheria na taratibu zilizowekwa pamoja na nyingine ili kuepuka adhabu na kufukuzwa shule.

Walimu shuleni ni waelekezaji, walezi, waelimishaji na washauri. Mwanafunzi akiwasikiliza atafika kule anakotarajia, alikopanga afike.

Mtu hawezi kudai kuwa ameelimika wakati hana tabia inayokubalika katika jamii yake. Licha ya elimu yake mtu huyo atakuwa msungo!

Jina ……..saini……..tarehe…….

KIAMBATISHO D.

THE UNITED REPBRIC OF TANZANIA
PMO-REGINAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

KWEMARAMBA SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 103,
LUSHOTO.
7/07/2018.

REF No KMSS A. 3/VOL 3./1 JUL.
TO MEDICAL OFFICER.
……
…….
……

REF: A PUPIL'S MEDICAL EXAMINATION FORM

Please Examine pupil……in respect of these areas and any other areas(S) deemed fit please. Which applies.

Does the pupil have problems in connection with……?.

(a) Sight Yes/No. If yes, state…….

……

(b). Hearing Yes/No If yes, state……
……

(c). T.B. or any other chronic Diseases. Yes/No If yes, state…….
……
……

(d) Blood pressure. Yes/No If yes, state……
……
(e) Any physical impairment(s). Yes/No If yes, state……
……

Do You therefore recommend this pupil to pursuer studies at this school ?.
……
……
……
…….

Name……..signature……date……
Official title…….Official stamp